



LIDA Stories

lidastories.net

Kuja Norwei / Å komme til Noreg

Aamiina

Julie Cornelia van Walsum

Jacob Haule (sw), Espen Stranger-


Johannessen (nn)



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>

Kuja Norwei

Å komme til Noreg



Aamiina

Julie Cornelia van Walsum

Jacob Haule

5

Kiswahili / nynorsk



Mimi na kaka zangu wawili tulikuja Norwei mwezi Disemba 2016. Tulivaa nguo za majira ya joto kwa sababu tulifikiri Norwei kutakuwa na joto kama Somalia. Hata hivyo, tulipofika uwanja wa ndege kulikuwa na theluji. Tulihisi baridi na hali ya hewa ilikuwa ya baridi sana. Ingawa tulibeba mabegi, yalikuwa na nguo za majira ya joto tu.

...


Dei to brørne mine og eg kom til Noreg i desember 2016. Vi hadde på oss sommarklede fordi vi trudde det ville vere like varmt i Noreg som i Somalia. Men då vi kom til flyplassen, snødde det. Vi fraus og vêret var kaldt. Sjølv om vi hadde med oss nokre koffertar, inneheldt dei berre sommarklede.



Hata kama kulikuwa na baridi, nilifurahi sana
tulipokuja Norwei. Hatimaye niliweza kufanikiwa
kuonana tena na mama yangu ambaye
sikumuona kwa miaka sita. Tulionana na mama
pamoja na rafiki zake wawili. Tulipomuona tulilia
kwa furaha. Tulienda kwenye mji mdogo
ambapo mama anaishi.

...


Sjøl om det var kaldt, var eg veldig glad då vi
kom til Noreg. Eg kunne endeleg møte mamma
att, som eg ikkje hadde sett på seks år. Mamma
og to av venninnene hennar møtte oss. Då vi
møtte mamma att, gret vi av glede. Mamma bur
i ein liten by, så vi køyrde dit.



Siku za mwanzo tukiwa katika mji wa mama zilikuwa ni za kustaajabisha. Kulikuwa na baridi na theluji na hatukuweza kuona chochote. Mitaa ilikuwa tupu kabisa. Watu wachache niliokutana nao walionekana wakihihi baridi na hawakuwa sawa. Somalia kulikuwa na watu kila mahali, kwa hiyo kila kitu kilikuwa kigeni hapa. Mama yangu na rafiki zake walitupatia zawadi na kisha akatupeleka kununua nguo za majira ya baridi.

...


Dei første dagane i byen til mamma var veldig merkelege. Det var kaldt, det snødde og det var lite å sjå. Gatene var heilt folketomme. Dei få personane eg møtte, verka kalde og uvennlege. I Somalia er det folk overalt, så alt kjendest uvant her. Mammaa mi og venninnene hennar gav oss gåver, og ho tok oss med for å kjøpe vinterklede.



Kama ningebaki Somalia, ninadhani ningekuwa mama mpaka sasa. Pengine ningekuwa na watoto wengi. Kama ningekuwa Somalia, nisingekuwa na fursa sawa kama nilizopata mpaka sasa. Ninajihisi mwenye bahati kuishi Norwei.

...


Viss eg framleis hadde budd i Somalia, hadde eg kanskje vore mor no. Kanskje eg hadde fått mange barn allereie. Viss eg hadde vore i Somalia, ville eg ikkje hatt dei same moglegheitene som eg har fått no. Eg føler meg heldig som bur i Noreg.



Baada ya mapumziko ya krismasi, nilijiunga na kozi ya kinorwei katika kituo cha elimu ya watu wazima. Nilisoma pale kwa muda wa miaka miwili kabla ya kuanza shule ya msingi. Sasa nipo mwaka wa mwisho na nimejitengezea marafiki wengi. Ninapenda sana kuongea na watu na kufurahia kuonana na watu wapya.

...

Efter juleferien byrja eg på norskkurs på vaksenopplæringsenteret. Eg gjekk der i to år før eg byrja på ein vanleg skule. No går eg siste året, og eg har fått mange nye venner. Eg er veldig sosial og eg er glad i å møte andre.



Mwaka ujao, nitaanza shule ya sekondari katika idara ya afya na maendeleo ya vijana. Hapo baadaye, ninataka kuwatumikia vijana. Nikimaliza elimu yangu, ndoto yangu ni kupata ajira ya kudumu. Pia ninataka kujifunza udereva na nipate leseni yangu ya udereva.

...


Neste år skal eg byrje på helse- og oppvekstfag på vidaregåande skule. I framtida vil eg bli barne- og ungdomsarbeidar. Når eg er ferdig med utdanninga mi, drøymmer eg om å få meg ein fast jobb. Eg vil òg lære å køyre bil og ta førarkort.



Baada ya masomo, huwa ninaenda kwenye kituo kinachoendeshwa na wajitoleaji ambapo huwa ninasaidiwa kufanya kazi ya nyumbani. Pia nimejiunga na kozi ya kushona katika kituo hiki.

...

Etter skulen drar eg til Frivilligsentralen for å få hjelp med leksene. Eg har òg byrja på eit sykurs der.



Nilipokuwa Somalia, sikuwahi kwenda shule au kujiunga na kozi yoyote isipokuwa shule ya Kuran. Sikujua kusoma wala kuandika. Sasa nimeshajifunza namna ya kuandika Kisomali na Kinorwei na masomo mengine mengi. Bila elimu, nilijihisi si kitu. Sasa ninajiona mwenye maarifa na furaha.

...

I Somalia fekk eg aldri moglegheit til å gå på skule eller ta eit kurs, bortsett frå koranskule. Eg kunne ikkje lese eller skrive. No har eg lært å skrive på både somali og norsk, og mange andre fag. Utan utdanning følte eg at eg ikkje var nokon. No føler eg meg kunnskapsrik og glad.